**JAMHURI YA MUUNGANO WA TA NZANIA**

**WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA**

**UMOJA WA SHULE ZA KIJESHI TANZANIA**

**MUONGOZO WA USAHIHISHAJI MTIHANI WA UTIMILIFU (MOCK) 2026**

**015 ELIMU YA DINIYA KIISLAMU**

**KIDATO CHA NNE**

**SEHEMU A (Alama 16)**

**1:**

| i | ii | iii | iv | v | vi | vii | viii | ix | x |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| B | D | A | C | B | D | A | E | A | B |

**2:**

| i | ii | iii | iv | v | Vi |
|---|---|---|---|---|---|
| E | G | A | D | F | B |

**SEHMU B(Alama 54)**

3: Hoja sita(6)zinazothibitisha kuwepo Allah(SW)kupitia historia ya maisha ya mwanaadamu.

i)Kuangamizwa watu wa (kaumu ya) A'd(Nabii Hud (as):

Watu hao waliongoza kwa teknolojia ya kujenga majumba marefu na walikuwa ni wenye nguvu.Allah(SW) aliwaangamiza kwa upepo mkali na hatimae Nabii Hud(as) na waumini wachache waliokolewa na Allah(SW)

ii)Kuangamizwa watu waThamud (Nabii Salih)(as):Watu hao walikataa ujumbewa Nabii Salih(as) kwa kumuua ngamia wa miujiza .Allah(sw) aliwaangamiza kwa tetemeko la ardhi lililosababishwa na ukulele wa Malaika.

iii)kuangamizwa watu wa Luti (as) .Allah (sw) aliwaangamiza makafiri hao kwa mvua ya changarawe (mawe) za motoni , kila kijiwe na mtu wake kasha ardhi iligeuzwa juu chini chini juu.

iv)kuangamizwa kwa Firauni (la) na majeshi yake: Firauni (la) na jeshi lake wali angamizwa katika bahari ya sham kwa kumezwa wote na maji isipokuwa mwili wa Firauni (la) ulitemwa na kueleya majini ili iwe funzo kwa wanaadamu wote.

v)kuangamizwa watu wa nabii Nuhu (as). Allah (sw) aliwaangamiza watu hao waliokuwa na nguvu na mamamlaka katika jamii zao kwa gharka ya maji.

vi)kuangamizwa kwa jeshi la Abraha,Gavana wa Yemen: Abraha aliandaa jeshi kubwa la askari na tembo walio funzwa vizuri kwa ajili ya kwenda kuibomoa Al-kaaba watu hao walisambaratiswa na jeshi dogo lililo dhaifu la ndege

vii)kufutika na kutoweka viongozi na wafalme maarufu duniani. Mfano Hitler, Mussolini na wengineo .Hoja 6 @ 1 =$01\frac{1}{2} \times 6 = 09$.

4:Haki sita za watumwa katika Dola ya kiislam.

i)watumwa walikuwa na haki ya uamini na kufuata mila au dini waipendayo bila kushurutishwa.

ii)wanapata huduma za kijamii kama malazi mavazi na chakula sawa na mabwana au wanaadamu wengine.

iii)walikuwa wakikosea wakisamehewa badala ya kuadhibiwa.

iv)mtumwa alistahiki kuwa kiongozi na kutiiwa ipasavyo maadamu ni muislamu na mcha mungu.

v)watumwa walikuwa na haki ya kujikomboa na kuwa huru.

Hoja sita @1= $01\frac{1}{2} \times 6 = 09$

5)Aina tatu za makosa na mfano wake.

i)kosa la hududi:Hududi ni makosa ambayo adhabu na hukumu zake zimeainishwa moja kwa moja katika Qur-an na sunnah ya mtume (saw). Mfano :mwizi hukumu yake akatwe mkono wa kulia.

ii)kosa la Taaziri: Ni makosa ambayo hukumu na adhabu zake hazijatajwa moja kwa moja katika Qur-an na Sunnah za Mtume (S.A.W) bali hukumu hii ameachiwa jaji kwa kuidhinishwa na kiongozi wa kiislamu.

iii)kosa la kisasi: Ni makosa ambayo yanampa mdhulumiwa haki ya kulipa kisasi kwa aliyemdhulumu. Mfano kuua au kujeruhi.

Hoja 3 @ 1 = $03 \times 3 = 09$.

6)Hoja sita (6) za kuonesha umuhimu wa mirathi katika uislamu.

i)Ni amri au agizo la Allah (sw)

ii)Ni utambulisho wa Imani na ucha mungu wa mtu.

ii)Kuacha na kukataa kugawa na kugawana mirathi kiislamu ni moja wapo ya sababu zitakazowapelekea watu kuingia motoni.

iv) Kugawa mirathi ni miongoni mwa sababuzitakazowafanya waumini waingie peponi.

v) Mrithi na mrithisishaji mkuu ni Allah(sw).

Mwenye kukanusha mirathi ametoka katika uislamu.

Hoja sita @1= $01\frac{1}{2} \times 6 = 09$

7)Mafunzo sita (6) yotokanayo na hija ya kuaga ya mtume Muhammad (saw) kwa jamii ya waislamu wa leo.

i)Waislamu wanapaswa walinde uhai wao, mali zao na heshima zao kwa gharama yoyote

ii)Kila mtu atalipwa kutokana na matendo yake.

iii)Waiisalamu wote ni ndugu. Hivyo hatupaswi kuoneana.

iv)Waislamu tusudhulumu haki za watu na tusikubali kudhulumiwa.

v)Waisalamu tupaswa kumcha Allah (sw).

vi)Waisalamu wanaume wanawajibu wa kuwatendea wema wake zao.

vii)Kiongozi wa kiisalamu anapaswa kutiiwa anapoamrisha mambo mema.

viii)Waisalamu tunapaswa kuifuata Qu-an na sunna katika kuendesha maisha yetu ili tusipotee na kupata hasara mbele ya Allah (sw).

ix)umuhimu wa kurejesha amana kwa wenyewe.

x)Waislamu wanapaswa wajiepushe na riba.

xi)Waisalamu wanapaswa kujiepusha na zinaa.

Hoj sita 6 @ = $01\frac{1}{2} \times 6 = 09$.

8) Sababu tatu (3) zilizo pelekea uasi (Riddaa) wakati wa khalifa Abubakar (ra)

i)Udhaifu wa Imani:Hii ilipelekea  watu kuacha zaka na wengine kutoa zaka lakini kwajamaa zao wa karibu na kushindwa kupeleka baitulmali.

ii)Kulinda uchumi wao, hadhi zao na nafasi zao .Hii ilikuwa kwa wale wasio waislamu walikuwa wakilipa jiz-ya.

ii)Kulinda utukufu wao :Hawa ndio wale walio rudi katika dini zao za awali na wengine kujitangaza utume katika miji yao na makabila yao.

**SEHEMU C** (alama 30)

9)Hoja nne namna ya kuiendea Qur-ani

i)Tupitie kwa makini maelezo ya kitabu hichi ili  tuwe na yakini kwa Qur-an ni kitabu cha Allah (sw) kisicho nashaka.

ii)Kwa kuwa na yakini      Qur-an ni ujumbe kutoka kwa Allah (sw), hatuna budi kuisoma kwa mazingatio na kujitahid kupata ujumbe unaotokana na kila aya.

iii)Ili kuupata  kwauwazi ujumbe wa kila aya au sura ya Qur-an hatuna budi kusoma tafsiri nasherehe za wanazuwoni mbali mbali waliojitahidi kuitafsiri Qur-an katika lugha tunayoimudu.

iv)Baada ya kuupata kwa uwazi ujumbe wa Qur-an hatuna budi kuyaingiza maagizo ya mola wetu katika utendaji hukmu  tukimfanya mtuume (sw) kiongozi chetu.

v)Ili kuingiza Qur-an yote katika maisha yetu ya kila siku na kujipamba na tabia ya Qur-an ni lazima tujenge tabia kuwa wasafiri wa Qur-an kuanzia sura ya kwanza hadi ya mwisho.

vi)Tufanye juhud ya kusimamisha uislamu katika jamii kwa mali zetu na nafasi zetu ili tuweze kufuata uislama wote katika kila kipenge cha maisha ya binafsi na ya jamii.

10)Hoja nne(4) kulikuwa na hitajio kubwa la uwandishi wa hadithi za mtume (saw) kipindi cha maswahaba.

i)Hadithi ni taarifa juu ya tabia na mwenendo wa mtume (saw) katika kuetenda, kukataza, kuamrisha au kuridhia jambo .

ii)Hitajio la kuendesha dola ya kiislamu katika maeneo mbali mbali kwa mujibu wa Qur-an na hadithi za mtume (sw).

iii)Makhalif wane waongofu, waliongoza dola ya kiisalamu kwa mujibu wa Qur-an na sunna kwa kutoa hukumu mbali mbali.

iv)Matatizo yakisiasa. Kuzuka ugomvi baina ya Ali (ra) na muaawiya (ra) na waislamu kugawanyika makundi makundi na watu wakaanza kutumia hadithi za mtume (saw) vibaya kulingana na matashi ya vkundi vyao.

v)Kuepusha uwezekano wa kuzuka hadithi za uongo. Kwa kuwa dola ya kiislamu ilikuwa imepanuka sana hivyo ulikuwepo uwezekano mkubwa wa kuzusha hadithi za uongo.

vi)Kuporomoka kwa dola ya kiislamu na kuibuka tawala za kifalme, hivyo zilizukz hadithi za uongo. Maadui wa uislamu walitumia mwanya huo kuzusha hadithi za uongo ili kutowa watu katika mafundisho sahihi ya uislamu.

vii)Kwa kuwa hadithi za mtume (saw) zinatumika katika kuendesha maisha ya muislamu zilistahiki kuhifadhiwa katika maandishi kwa ajili ya watu wote wa nyakati zote.

11)Faida sita(6) za kutekeleza ibada ya hija.

i)Hutoa fursa ya mahujaji kuangalia pamoja mustakbali wao wa kuongoza na kusimamisha uadilifu ulimwenguni.

ii)Hutoa fursa ya kukumbusha juu ya mkutano wa siku ya malipo ambapo watu wote watahudhuria ili walipwe kulingana na matendo yao duniani.

ii)Huwawezesha watu kujua, kupenda , na kusaidiana katika kutatua matatizo juu yakila hali.

iv)Huimarisha umoja na udugu baina ya wanadamu wote.

v)Huimarishika mshikamano wa waislamu katika jamii.

vi)Huimarisha usawa baina ya wanadamu wote.

vii)Huwawezesha waislamu kuweka mikakati na mbinu za kuupeleka mbele uislamu.

viii)Huwawezesha waislamu kupanga namna ya kukabiliana na changamoto mbali mbali zinazo ikbili jamii yao.

ix)Huwawezesha waislamu kufanya tathmini ya uislamu kidunia.

Utangulizi alama $01\frac{1}{2}$.

Kiini: Hoja sita 6 @ alama $02 \times 6 = 12$

Hitimisho alama $01\frac{1}{2}$. Jumla 15.